

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA



## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga anapenda kuwatangazia watazania wote wenye sifa nafasi za kazi ili kuboresha utendaji kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kwa ufanisi zaidi.

### 1.0 Mtendaji wa Kijiji III – (Nafasi 40)

#### **2.1 Ngazi ya Mshahara: TGS B**

#### **2.2 Majukumu ya kazi:**

- (i) Mtendaji wa Shughuli zote za Kijiji.
- (ii) Mtunzaji wa kumbukumbu zote za kijiji za vikao vya Kijiji pamoja na hati ya kuandikishwa Kijiji, mali za kijiji, na rejesta ya kijiji.
- (iii) Kuhamasisha utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya Kijiji.
- (iv) Mlinzi wa amani katika Kijiji.
- (v) Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo katika Kijiji.
- (vi) Kupanga na kuhakikisha kupitishwa kwa ratiba za vikao vya mkutano mkuu na Halmashauri ya Kijiji.
- (vii) Kuandaa taarifa mbalimbali za Halmashauri ya kijiji kwa ajili ya mkutano mkuu wa kijiji.
- (viii) Msimamizi wa mapato na kodi za kijiji.
- (ix) Mfuatiliaji wa miradi ya kijiji na kutoa taarifa kwenye halmashauri ya kijiji.

## **2.3 Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe Mtanzania
- (ii) Awe mhitimu wa kidato cha nne au cha sita mwenye cheti cha fani ya Utawala, Sheria, Rasilimali watu, Maendeleo ya jamii au usimamizi wa fedha kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- (iii) Awe na Umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

### **MAELEKEZO YA JUMLA**

1. Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya Elimu na Taaluma yake.
2. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Andika nafasi uliyoomba juu ya bahasha yenye barua yako ya maombi.
4. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/09/2017 saa 9:30 alasiri.
5. Tangazo hili linapatikana pia kupitia tovuti: [www.mkingadc.go.tz](http://www.mkingadc.go.tz)
6. Maombi yatakayowasilishwa moja kwa moja na mwombaji kwa mkono hayatafanyiwa kazi.
7. Maombi yote yatumwe kupitia anwani ya :

**MKURUGENZI MTENDAJI(W)**

**S.L.P 6005,**

**TANGA.**